# SHERIA NDOGO ZA

# HALMASHAURI YA

# WILAYA YA URAMBO

# ZA MWAKA 2012

ISSN 0856 – 034X

*Supplement No. 17* *11th May, 2012*

# *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 19 Vol. 93 dated 11th May, 2012*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 156 la tarehe 11/05/2012

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (I) na 16 (I))*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO YA MISITU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2012

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, 2012 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu), 1996 za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ambazo zitaitwa Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

2. Sheria Ndogo Kuu linafanyiwa marekebisho kwa kuongeza viwango vya ushuru kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi:-

3. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha makosa na adhabu kwa kuongeza makosa ya wakala ambacho kitasomeka kama ifuatavyo:-

Wakala yeyote aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi ambaye;-

(a) atashindwa kukusanya kiasi cha ushuru alichokadiriwa na Halmashauri;

(b) atashindwa kuwasilisha kwa Halmashauri kiasi cha ushuru alichokusanya:

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI

| *Na.* | *Mazao* | *Aina ya Mazao* | *Kiasi cha Ushuru* |
|---|---|---|---|
| 1. | Mpingo | Gogo | 800/= kwa kila gogo |
| 2. | Mninga | Silipa | 800/= kwa kila silipa |
| 3. | Mkasanda | Gogo | 800/= kwa kila gogo |
| 4. | Mkola | Silipa | 800/= kwa kila silipa |
| 5. | Mkasanda | Gogo | 800/= kwa kila gogo |
| 6. | Mkola | Silipa | 800/= kwa kila gogo |
| 7. | Mfundu | Silipa | 800/= kwa kila gogo |
| 8. | Mzinga | Mbao | 200/= kwa kila mbao |
| 9. | Mtundu | Mbao | 200/= kwa kila mbao |
| 10. | Mkaa | Gunia | 100/= kwa kila gunia |
| 11. | Rafia | Mondo (Fibre) | 100/= |
| 12. | Gundi | | 200/= |
| 13. | Asali | | 1000/= kwa kilo |
| 14. | Kibali cha Kuingia kwenye msitu kwa shughuli mbalimbali | | 1,500/= |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 157 la tarehe 11/05/2012

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA 287)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa Afya, Daktari wa Wilaya, Afisa Afya msaidizi, Afisa Mtendaji Kata, Mkuu wa Masoko na Afisa yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa hii ni pamoja na:-

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula.

(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula.

(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari n.k.)

"Choo" maana yake ni chumba maalum ambacho kimejengwa na kwa ajili ya kuhifadhi kinyesi cha binadamu.

"Eneo lililo wazi" maana yake ni eneo lililochini ya Halmashauri ya Manispaa ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

"Kero" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali

yoyote au kinatumika, au kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

(a) hatari kwa viumbe au maisha ya wanadamu;

(b) harufu mbaya yenye kuudhi;

(c) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, inzi, panya na viumbe wenye madhara.

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Majani" maana yake ni majani yote marefu, vichaka vyenye urefu wa sentimeta 15 au zaidi vinavyopatikana sehemu yeyote ndani ya Halmashauri ya Manispaa, hii ni pamoja na mazao marefu yanayolimwa kando ya barabara.

"Maji taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani;

"Mabomba ya maji machafu" maana yake ni mabomba yanayotumika kuchukua maji machafu kutoka majumbani au kwenye mifereji ya maji machafu au ya mvua ni pamoja na bomba lolote lililo wazi linaloweza kupitisha maji machafu au ya mvua.

"Taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka;

"Usafi wa Mazingira" maana yake ni usafi wa mazingira yanayozunguka binadamu kuwa katika hali isiyoweza kuleta madhara kwake na wengine, hii ni pamoja na Maji, Miti, hewa, ardhi na wanyama pamoja na viumbe visivyo hai kama vile nyumba.

"Vyanzo vya maji" maana yake ni maziwa, mabwawa, visima vya aina zote chemichemi na mito.

Wajibu wa wakazi

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mwenye nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba:-

(a) mazingira yanayozunguka eneo la nyumba yake

yanakuwa safi wakati wote.

(b) takataka au uchafu wowote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri.

(c) anajenga choo imara chenye upana wa futi 4 kwa 4 kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati au nyasi na kinachotumika muda wote.

(d) anaifanyia nyumba yake matengenezo mara moja inapokuwa imeharibika.

(e) eneo lake analofanyia biashara liko katika hali ya usafi.

(f) eneo linalomzunguka halina mazalia ya mbu.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumwaga takataka za aina yoyote katika Mtaa, uchochoro au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa na kufanya usafi katika eneo lake mara kwa mara.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

5. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote ndani ya Halmashauri ili kukagua kama kuna kero yoyote na kumtaka mtu anayehusika na kero hiyo kuiondoa katika muda atakaopewa na Afisa Mwidhiniwa.

Wajibu wa wahudumu kupima afya

6. Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, au watu wanaoshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba wanapima afya zao mara moja kila baada ya miezi sita pamoja na kuwa na kibali cha Halmashauri kinachomruhusu kuendesha biashara hiyo.

Maji taka

7. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha shimo la maji machafu wazi au kumwaga maji, au taka, kutapisha ama kuruhusu kumwaga au kutapisha au kuruhusu kufurika choo, karo, septic tank, soakage pit, cepool, au kuruhusu kupasuka au kuziba bomba la maji taka toka ndani ya nyumba na kuyatiririsha kwenye barabara, njia, kichaka, eneo la burudani ama sehemu nyingine isiyokusudiwa.

Wajibu wa kutoa taarifa za magonjwa au na vifo

8.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu atakayekuwa na habari au mashaka ya mtu kuugua ugonjwa usiokuwa wa kawaida au ugonjwa unaosababisha kifo kutoa taarifa kwa Mkurugenzi au Mganga Mkuu au Afisa aliyeidhinishwa.

(2) Baada ya kupokea taarifa za ugonjwa Mkurugenzi au Mganga Mkuu anaweza kutoa amri ya kuondoa watu wote katika nyumba ambayo ugonjwa huo umetokea, au kunyunyizia dawa za kuulia viini vya magonjwa, au kupulizia dawa au kuharibu vitu endapo itaonekana kwamba vitu hivyo vina viini vya magonjwa.

(3) Endapo itathibitika kuzuka kwa ugonjwa wa mlipuko Mkurugenzi atamtaarifu Mkuu wa Wilaya juu ya kuzuka kwa Ugonjwa huo, na Mkuu wa Wilaya anaweza kutoa amri ya Maandishi juu ya namna ya kuzuia na kudhibiti ugonjwa huo usienee.

Kupiga kelele

9. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia muziki kwa sauti ya juu ambayo itasababisha makelele na kuwa kero kwa wakazi wengine.

Upikaji na uuzaji wa chakula

10.-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuzuia upishi, na uuzaji wa vyakula katika mazingira yasiyoridhisha kiafya.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza au kuuza chakula mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za Afya na awe amepata kibali kutoka Halmashauri.

Makosa

11. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote:-

(a) kujenga choo umbali wa mita 30 kutoka kisimani, ziwani, mtoni au chanzo kingine cha maji yanayotumika kwa matumizi ya binadamu.
(b) kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu, na kuyatiririsha kwenye barabara, mitaa au kwenye mifereji ya maji ya mvua au mfereji wowote ulio wazi.
(c) kutupa takataka au kusababisha mtu mwingine atupe takataka au kusababisha mrundikano wa takataka mahali popote palipokatazwa na Halmashauri.
(d) kutiririsha maji machafu yanayoweza kusababisha kero kwa wakazi wa maeneo husika.
(e) kuuza chakula nje ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutimiza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi 12 jela au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyozidi shilingi laki tatu mtu yeyote endapo mkosaji atakiri kutenda kosa hili kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoonyeshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2011

Mimi..............................Nakiri mbele ya ...............................Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwamba mnamo tarehe........................ ya mwezi..........mwaka........Nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha............Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2011. Nipo tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi atatekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe..............................          Sahihi................................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

L.S

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 158 la tarehe 11/05/2011

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*Zimetungwa chini ya kifungu Na. 7(1) na 16 (1)*

---

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;-

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

"Kibali" maana yake ni hati inayotolewa na Halmashauri kwa mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni, shirika au taasisi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uchimbaji, utafiti, usafirishaji, au biashara ya madini ya ujenzi;

"Madini ya ujenzi" maana yake ni mchanga, mawe, kokoto chokaa pamoja na madini yoyote ambayo sio vito vya madini;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Ushuru" maana yake ni malipo ya fedha yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi.

Ushuru

3.-(1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa madini ya ujenzi kutoka kwa kila mnunuzi wa madini hayo katika eneo la

Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru huo utalipwa kwa Halmashauri au Wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo kuthibitisha malipo hayo.

Tathimini ya athari kwa mazingira

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mchimbaji wa madini ya ujenzi mwenye kibali kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa mujibu wa sheria na kanuni za mazingira zilizopo hapa nchini kabla ya kuchimba madini hayo.

Kibali

5.-(1) Mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au shirika wanaotaka kujishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi atatakiwa kuwa na kibali cha Halmashauri kinachomruhusu kufanya hivyo.

(2) Baada ya kufanya uchunguzi endapo uchimbaji huo hauna athari kwa mazingira na wakazi wa eneo yanapochimbwa madini hayo Halmashauri itatoa kibali cha kuruhusu uchimbaji wa madini hayo kitakacholipiwa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(3) Kibali kitakachotolewa na Halmashauri kitaeleza aina ya Madini yanayochimbwa na eneo yatakapochimbwa madini hayo.

Kuwasilisha taarifa za mapato

6. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika linalojishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi kutoa taarifa ya mapato yake ya mwaka au mwezi kama itakavyoelekezwa kwa Halmashauri.

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa

7. Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote zinapofanyika shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi wakati wa saa za kazi kwa lengo la kufanya ukaguzi na kukusanya takwimu sahihi za uchimbaji wa madini unaofanyika katika eneo hilo.

8. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au shirika kununua, kuuza, kutafiti, kuchimba au kusafirisha madini ya ujenzi bila kuwa na kibali cha Halmashauri.

9. Mtu yeyote ambaye ataficha vitabu au nyaraka nyingine za fedha, au atatoa takwimu au taarifa za uongo kuhusu mapato ya mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au shirika linalojishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Makosa na adhabu

10. Mtu yeyote, Shirika au Kampuni itakayokwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifili-sha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

Malipo ya kibali

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha kuchimba na kuuza mawe, mchanga. | 100,000/= |
| 2. | Kibali cha kuchimba udongo | 500,000/= |
| 3 | Kibali cha kuchimba chokaa | 500,000/= |
| 4 | Kibali cha kuchimba kokoto | 200,000/= |
| 5 | Kibali cha kuchimba madini mengine | 100,000/= |

## JEDWALI LA PILI

Kiwango cha ushuru unaotozwa

| *Na.* | *Aina ya Madini* | *Tani* | *Shilingi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Mawe kwa ajili ya kutengeneza chokaa | 1 | 3000 |
| 2. | Changarawe | 1 | 3000 |
| 3. | Udongo kwa ajili ya shughuli yoyote | 1 | 1,500 |
| 4. | Mawe kwa ajili ya Ujenzi | 7 | 1,500 |
| 5. | Mchanga | 7 | 1,500 |
| 6. | Chokaa na kifusi | 1 | 1,500 |

---

JEDWALI LA TATU

---

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2011.

HATI YA KUKIRI KOSA

*(Chini ya kifungu cha 11)*

Mimi.......................................nakiri mbele ya ..................................Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, kwamba mnamo tarehe ............ya mwezi .................. Mwaka ...................... nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ....................cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2011. Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza Mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe....................................Sahihi..............................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 159 la tarehe 11/05/2012

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini kifungu cha153*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

## SEHEMU YA KWANZA:

### UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa Vinginevyo:-

"Afisa mwidhinishwa" maana yake ni afisa maliasili, afisa kilimo na mifugo pamoja na afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Eneo la Hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo;

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na afisa mwidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote.

''Kiwanda'' maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa.

''Kuvuna misitu''maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti, visiki.

"Maeneo ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri.

"Maji" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi, na maji yaliyoko katika mkondo.

"Maji taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani.

"Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotasfiriwa katika Sheria ya Misitu na.14 ya mwaka 2002 chini ya kifungu Na. 2 ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la msitu.

"Mazingira" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 yanahusisha

maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za Kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana.

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mifugo" maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu.

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri

"Taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

"Taka Ngumu" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps).

"Taka za Viwandani" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana

yake ni Uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004 sehemu ya IX.

"Uchafu Hatari" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira.

"Uchafuzi wa Mazingira" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo moja kwa moja, joto, kemikali, biolojia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambao unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali ya hatari kwa afya ya jamii, usalama, au ustawi, au hatari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu, au kizuizi ambacho ni sehemu katika sheria hizi.

"Udongo" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi.

''Vitu hatari" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, ni kemikali yoyote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira.

''Waziri'' maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI

### MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi;-
   (a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoamriwa na Halmashauri.;
   (b) atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;
   (c) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia (stock routes) zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;
   (d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
   (e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na halmashauri;
   (f) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;
   (g) atatakiwa kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;
   (h) atatakiwa kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
   (i) atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;
   (j) atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajiwa na Halmashauri;
   (k) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o.

Masharti ya mfugaji

5. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote;
   (a) kuchunga, kulisha, au kunywesha maji mifugo katika maeneo ya mipango miji pamoja na maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;
   (b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
   (c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;
   (d) kibali cha kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri kitatolewa na afisa kilimo na mifugo;
   (e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoaidhinishwa na Halmashauri;

(f) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;

(g) Ni marufuku kwa mfugaji yeyote kupitisha mifugo; katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

6.-(1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote Utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama ilivyoainishwa hapa chini na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

| *Na.* | *Aina ya Mfugo* | *Kiasi cha Faini* |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 5,000/= |
| 2 | Mbuzi | 3,000/= |
| 3 | Kondoo | 3,000/= |
| 4 | Nguruwe | 2,000/= |

(3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(5) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) halmashauri itarudisha fedha zake.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

Ukaguzi wa mifugo

7.-(1) Itakuwa halali kwa afisa kilimo na mifugo, maafisa watendaji wa kata na vijiji, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au jengo lolote wakati wowote kwa

madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

(2) Mtu yeyote atakaye wazuia maafisa waidhinishwa katika kifungu cha 7(1) kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

8.-(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo maalumu Kwa ajili ya shughuli za malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 pamoja na Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na.20 ya Mwaka 2004.

(2) Halmashauri itatenga njia maalumu ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au Minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9.-(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia nyama mahali pengine popote.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya Biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

## SEHEMU YA TATU
### KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

Taratibu za kilimo

10.-(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia sheria

ya Ardhi sura ya 113 na 114 na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.

(2) Itakuwa halali kwa Afisa kilimo kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Masharti kwa mkulima

11.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka kwa Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4.00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za Kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia Kilimo cha kuhamahama na kuhimiza Kilimo cha mzunguko (crops rotation).

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

14. Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

SEHEMU YA NNE

HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

15.-(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itakuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

kulinda eneo la hifadhi

16.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji Kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

17.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote, Kiwanda, Taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni Chanzo cha Maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

SEHEMU YA TANO:

HIFADHI YA MISITU

Kuchoma au kusababisha moto

18.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika Misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, Kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto

19. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto.

Ukataji miti

20.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wajibu wa kupanda miti

21. Kila Mkazi wa Halmashauri atawajibika-

(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake;

(b) kupanda na kutunza miti katika makazi yake;

(c) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

22. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji;

(a) kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye;

(b) kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la Kijiji;

(c) kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake;

(d) Mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti wa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo, itabidi apate kibali cha maandishi toka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji na kibali cha Afisa Maliasili wa Wilaya au Wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya;

(e) kila kijiji kitapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza;

(f) kila Shule au Taasisi nyingineyo Wilayani itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lisilopungua miti hekta 2;

(g) kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;

(h) kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo;

(i) kila mtu mwenye nyumba kwenye Mji Mdogo atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza;

(j) kila Mwenyekiti wa Kitongoji, Mtendaji wa Kijiji, Mkuu wa Taasisi yoyote Wilayani atahakikisha kuwa Kijiji au Taasisi ina msitu wa hifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingira na matumizi ya baadaye.

## SEHEMU YA SITA

### TAKA NGUMU NA LAINI

Utupaji wa taka ngumu na laini

23.-(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au Kujisaidia katika kingo za maziwa, mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa viwanda

24. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda Kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha Uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

## SEHEMU YA SABA

### MAKOSA NA ADHABU

Makosa yanayohusu mifugo

25. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa;

(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(b) atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali;
(c) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;
(e) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo (kokoro).

Makosa yanayohusu kilimo

26. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu kuhifadhi ardhi

27. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi Ardhi atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu vyanzo vya maji

28.-(1) Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu kuharibu misitu

29. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa;
- (a) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali; au,
- (b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto; au
- (c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali; au
- (d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali; au
- (e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;
- (f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;
- (g) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;
- (h) atabandua magome ya miti kwa ajili kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali;
- (i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini

30. Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa na Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu taka za majimaji

31. Mtu yeyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu viwanda

32. Mtu yoyote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa

nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.

33. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300, 000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

L.S

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 160 la tarehe 11/05/2012

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
SURA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA YA LESENI ZA UVUVI NA VYOMBO VYA UVUVI) MAREKEBISHO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2012

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada ya Leseni za Uvuvi na Vyombo vya Uvuvi) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Urambo, za mwaka 2012 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada ya Leseni za Uvuvi na Vyombo vya Uvuvi) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 1988 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Tangazo la serikali Na 110 la tarehe 25/7/1989

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiasi cha ushuru kinachotozwa kama inavyoonekana kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

3. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwenye kifungu cha adhabu kitakachosomeka:-

"Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

4. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu cha kufifilisha kosa kitakachosomeka:-

"Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa".

JEDWALI LA KWANZA

| *Na.* | *Aina ya Chombo au Mvuvi* | *Aina ya Uvuvi na Ada ya Kibali* |
|---|---|---|
| 1 | Mvuvi asiye na chombo | Sh 1,000/= kwa mwaka |
| 2 | Kusafirisha mlimba mmoja wa samaki kwenda popote ndani ya wilaya. | Sh 1,500/= kila mlimba |
| 3 | Mbanishi wa samaki | Sh 1,200/= kila mwaka |
| 4 | Mvuvi wa kokoro mwenye chombo chenye injini au kisicho na injini. | Sh 2,000/= kwa mwezi |
| 5 | Mvuvi wa chombo cha injini | Sh 2,000/= kwa mwaka |
| 6 | Ada ya uandikishaji chombo kisicho cha injini | Sh 1,200/= kwa mwaka |
| 7 | Ada ya uandikishaji chombo chenye injini | Sh 1,500/= kwa mwaka |
| 8 | Kusafirisha samaki au zao la samaki toka eneo la kuvulia hadi sehemu ya kusafirishia:-<br>(a) Kutumia gari au trekta kusafirishia samaki.<br>(b) Kutumia baiskeli kusafirishia samaki. | <br><br>Sh 2,000/= kwa mwaka<br>Sh 1,500/= kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

SHERIA NDOGO ZA (ADA YA LESENI ZA UVUVI NA VYOMBO VYA UVUVI) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2011.

HATI YA KUKIRI KOSA

*(Chini ya kifungu cha 11)*

Mimi.............................................. nakiri mbele ya ................................. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, kwamba mnamo tarehe ...........ya mwezi..................mwaka...........................nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ...................cha Sheria Ndogo za (Ada ya Leseni za Uvuvi na Vyombo vya Uvuvi) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2011. Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza Mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe..................................... Sahihi...............................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

L.S

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 161 la tarehe 11/05./2012

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
SURA 287

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA (KUHIFADHI VYANZO VYA MAJI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA URAMBO ZA MWAKA 2012

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kuhifadhi Vyanzo vya Maji na Utunzaji wa Mazingira) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Urambo, za mwaka 2012 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Kuhifadhi Vyanzo vya Maji na Utunzaji wa Mazingira) (Marekebisho), 1997 za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

TSN 332 la tarehe 25/7/1997

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwenye kifungu cha adhabu kwa kuongeza kiwango cha faini inayotozwa kwa mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizo kitasomeka kama ifuatavyo:

"Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi laki mbili (200,000/=) au kifungo kisichozidi miezi 3 au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo".

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 162 la tarehe 11/5/2012

# SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7 (1) na 16 (1).*

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012.

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa muidhiniwa" ina maana ya Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290;

"Hesabu" ina maana ya jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada, katika mwaka wa mapato;

"Hesabu za mwisho"ina maana ya hesabu za mwisho

zinazowasilishwa na Taasisi yoyote ya kibiashara baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa aya ya 9 ya Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizo;

"Jumuisho" ina maana ya taarifa, nyaraka au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho;

"Kipindi cha hesabu" ina maana ya muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mkusanya kodi" maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mwaka wa Mapato" maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

"Taasisi ya kibiashara" ina maana ya taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Makampuni au Sheria ya Majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Utozaji wa kodi

4. Halmashauri itatoza na kukusanya kodi ya huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutoka kwa kila taasisi ya kibiashara katika kila mwaka wa mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu ya shughuli zote

zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au huduma zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

Uwasili-shaji wa taarifa kuhusu shughuli za kibiashara

5. Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionesha kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kuingizwa, kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

Uwasili-shaji wa taarifa

6. Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mtu yeyote mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yoyote ya kibiashara inayopaswa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo.

Uwezo wa kuingia kwenye jengo

7. Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Muidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la Taasisi ya kibiashara au la mlipa au mkusanya kodi yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi au mkusanya kodi hiyo.

8.-(1) Mkurugenzi anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya Kodi ya huduma.

(2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya 8(1) Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhiniwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

Uwasili-

9. Kila mlipa au Mkusanya Kodi ya huduma atatakiwa

shaji

kutoa na, au kuwasilisha hesabu za awali na kulipa kodi anayotakiwa katika muda kama ifuatavyo:-

(a) kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa kodi katika muda kama itakavyokuwa imeelekezwa na Kamishina wa Kodi ya forodha na kodi ya mlaji;

(b) wazalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa kodi kama itakavyokuwa imeelekezwa na kamishna wa Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa Kodi ya mlaji au (VAT);

(c) watu wengine watalipa katika awamu nne (4) awamu ya kwanza ikianzia katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuanza kwa kipindi cha mahesabu.

Uteuzi wa mkusanya kodi

10. Mkurugenzi anaweza kuteua Kamishna wa Kodi ya forodha au kodi ya mapato kutathmini na kukusanya Kodi ya huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria Ndogo ya 9 kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata kodi pamoja na madeni yake.

11.-(1) Kiwango cha kodi kitakuwa ni Asilimia 0.3% ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

(2) Mkusanya kodi au mlipa kodi yeyote akishindwa kuwasilisha Kodi yake au ya mlipa kodi, atachukuliwa kama hajalipa kodi na anastahili au kuwajibika kulipa kodi hiyo kama vile ndiye mlipa Kodi ya Halmashauri, na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipa kodi husika.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kuteua wakala kukusanya kodi kwa niaba yake na wakala huyo atakuwa na jukumu la:-

(a) kuwasilisha majumuisho kwa Mkurugenzi au Afisa

muidhiniwa;

(b) kuwasilisha kodi aliyokusanya katika kipindi maalum.

12.-(1) Kila mlipa kodi au mkusanya kodi atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi minne tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anayostahili katika mkupuo mmoja.

(2) Mlipa kodi au mkusanya kodi anapowasilisha hesabu zake, Afisa muidhiniwa anaweza:-

(a) kupokea na kukubali hesabu hizo na kutathmini kodi katika msingi huo;

(b) kufanya tathmini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa kodi huyo iwapo atakuwa na hisia za kimsingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi.

(3) Iwapo mlipa kodi hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wowote wa pato aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa anafikiri kwamba mlipa kodi huyo ana wajibu wa kulipa kodi kwa mwaka huo, anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo, isipokuwa tathmini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa kodi anayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo.

(4) Kodi iliyotathminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, italipwa katika siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

13.-(1) Mtu yeyote anayetakiwa kulipa kodi akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi katika kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia 1.5 kwa mwezi au shilingi elfu hamsini kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa.

(2) Iwapo mtu yeyote atasema uongo au ataficha baadhi

ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa, na inapobainika kuwa ufichaji au upunguzaji huo aliufanya kwa makusudi, mtu huyo atatozwa ushuru pamoja na nyongeza ya kodi ya asilimia hamsini (50%) ya tofauti kati ya kodi anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha pamoja na kiwango cha kodi halisi.

Jumla ya riba kutozwa kwenye kodi isiyolipwa

14.-(1) Kodi ambayo haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia 15% kwa mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na kodi inayodaiwa.

(2) Riba itozwayo katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama kodi inayostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama kodi inayolipwa na mlipa kodi huyo.

Kushindwa kutimiza maagizo

15. Mtu yeyote ambaye bila ya sababu za msingi:-

(a) atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;
(b) atashindwa kuwasilisha Nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa;
(c) atashindwa kutunza kumbukumbu, kitabu au hesabu;
(d) atashindwa kuonyesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi:

atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utoaji wa taarifa ya uongo

16. Mtu yeyote bila ya sababu za msingi:-

(a) akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi;
(b) akitoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa kodi;
(c) akiandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au kumbukumbu;

(d) atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa Muidhiniwa

kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

atakuwa ametenda kosa.

Adhabu

17.-(1) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au atatumikia kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo ya 17(1), mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifili-sha kosa

18. Endapo mtu ametenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kushughulikia kosa hilo na kuagiza kuwa mtu huyo alipe deni analodaiwa kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi pamoja na adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini.

---

JEDWALI

---

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2011.

HATI YA KUKIRI KOSA

*(Chini ya kifungu cha 18)*

Mimi.......................................nakiri mbele ya .................................. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, kwamba mnamo tarehe ............ya mwezi...................mwaka.......................nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ...................cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2011. Nipo tayari kulipa

kiasi cha faini ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza Mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 18 cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.................................Sahihi.............................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti, 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S.

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI,

MHE MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

DODOMA,
21 Aprili, 2012

TANGAZO LA SERIKALI NA. 178 la tarehe 18/05/2012

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Eneo la Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni mtumishi ye yote wa Halmashauri ambaye atateuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Gulio" maana yake ni eneo au sehemu yo yote ya wazi au iliyojengwa, na imetengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao ya shamba na bidhaa zingine za viwanda kwa siku maalum;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo;

"Mazao" maana yake ni pamoja na mazao ya chakula, mazao ya biashara na mazao ya misitu na maliasili ambayo kwa kawaida huzalishwa au kupatikana katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa ye yote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yo yote inayojishughulisha na ununuzi wa mazao katika eneo la Halmashauri kwa nia ya kufanya biashara;

"Muuzaji" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yo yote inayojishughulisha na uuzaji wa mazao katika eneo la Halmashauri.

Ushuru

4.-(1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa mazao kwa asilimia tatu ya bei ya mauzo ya soko kutoka kwa kila mnunuzi wa mazao kwenye eneo la Halmashauri.

(2) Ushuru huo utalipwa na mnunuzi kabla ya kusafirisha mazao.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi aliyelipa ushuru kuhakikisha anapewa stakabadhi ya malipo yaliyofanyika na atatakiwa kuionyesha kwa Afisa Muidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(4) Upimaji wa mazao utafanyika kwa mzani au kipimo cho chote kingine kilichothibitishwa na Halmashauri au mamlaka nyingine iliyowekwa kisheria.

(5) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi ye yote kupokea na au kusafirisha mazao ambayo hayajalipiwa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa mnunuzi

5.-(1) Kila mnunuzi wa mazao atatakiwa:-

(a) kununua mazao kwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kusaini mkataba na Halmashauri ambapo itamruhusu kununua zao husika kutoka kwa wazalishaji waliomo katika eneo la Halmashauri;

(c) kuwa na leseni halali ya biashara;

(d) kuwatambulisha rasmi wasaidizi wake kwa Halmashauri kabla ya kupewa kibali, na nakala halisi ya majina na picha za wasaidizi hao, ikiwa ni pamoja na sahihi zao itatuzwa na Halmashauri kwa kipindi chote cha msimu husika.

(2) Baada ya kusaini mkataba mnunuzi atapewa kibali cha kununua mazao kama kinavyoonyeshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(3) Mnunuzi ye yote anayedaiwa ushuru wa msimu uliopita atatakiwa kulipa deni lake kabla hajapewa kibali kwa ajili ya ununuzi wa mazao kwa msimu unaofuata.

Uuzaji wa mazao

6.-(1) Mazao yote yatauzwa katika magulio yaliyoainishwa na Halmashauri isipokuwa mazao ya maliasili na misitu ambayo yanaweza kuuzwa mahali pengine kwa kibali cha Halmashauri.

(2) Mzalishaji ye yote anayekusudia kuuzia mazao yake shambani au sehemu nyingine ambayo si gulioni atawajibika kuomba ruhusa kwa maandishi kutoka Halmashauri ndani ya miezi miwili kabla ya msimu wa mavuno ya zao husika.

Wajibu wa kutoa taarifa

7. Mkurugenzi kwa maandishi anaweza kumuagiza mnunuzi au mzalishaji ye yote kuandaa na kukabidhi taarifa ya kiasi cha mazao alichozalisha au kununua katika kipindi kinachotajwa katika agizo hilo.

Muda wa kusafirisha mazao

8. Itakuwa marufuku kuuza, kununua na kusafirisha mazao kabla ya saa kumi na mbili (12:00) alfajiri na baada ya saa kumi na mbili (12:00) jioni isipokuwa kwa ruhusa maalum ya maandishi itakayotolewa na Mkurugenzi.

Makosa

9. Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa iwapo:-

(a) atasafirisha mazao bila kulipa ushuru;

(b) kwa makusudi atamsaidia mnunuzi kukwepa kulipa ushuru;

(c) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru;

(d) atasafirisha mazao nje ya muda ulioainishwa;

(e) atanunua mazao bila kuwa na leseni.

Adhabu

10. Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

| *Na.* | *Aina ya mazao* | *Ushuru kwa asilimia* |
|---|---|---|
| 1. | Tumbaku | 5% |
| 2. | Pamba AR | 5% |
| 3. | Pamba BR | 5% |
| 4. | Maharage | 5% |
| 5. | Mchele | 5% |
| 6. | Alizeti | 5% |
| 7. | Karanga | 5% |
| 8. | Mahindi | 5% |
| 9. | Mpunga | 5% |
| 10 | Mhogo | 5% |
| 11. | Vitunguu | 5% |
| 12. | Nyanya | 5% |
| 13. | Mazao mengine ambayo hayajaainishwa | 5% |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti, 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S.

ADAMU MALUNKWI,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI,

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 179 la tarehe 18/05/2012

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 6(1))*

SHERIA NDOGO ZA (ADA YA UCHINJAJI NA UCHUNAJI (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada ya Uchinjaji na Uchunaji) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Urambo, za mwaka 2012 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada ya Uchinjaji na Uchunaji) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 1996 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwenye kifungu cha adhabu kwa kufuta kifungu hicho na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:

"Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu 50,000/= au kifungo kisichozidi miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo".

3. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika jedwali la kwanza, pili na tatu kwa kuongeza viwango vya ushuru kama ilivyoainishwa hapa chini na kufuta jedwali la nne na la tano

JEDWALI LA KWANZA

Ada ya machinjio

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Ng'ombe........................................ | 1,500/= | kwa kichwa |
| (ii) | Nguruwe........................................ | 1,500/= | kwa kichwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (iii) | Mbuzi.......................................... | 500/= | kwa kichwa |
| (iv) | Kondoo.......................................... | 500/= | kwa kichwa |

JEDWALI LA PILI

Ada ya ukaguzi wa awali

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Ng'ombe.......................................... | 1,000/= | kwa kichwa |
| (ii) | Nguruwe.......................................... | 1,000/= | kwa kichwa |
| (iii) | Mbuzi.......................................... | 500/= | kwa kichwa |
| (iv) | Kondoo.......................................... | 500/= | kwa kichwa |

JEDWALI LA TATU

Ada ya ukaguzi wa nyama

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Ng'ombe.......................................... | 1,000/= | kwa kichwa |
| (ii) | Nguruwe.......................................... | 1,000/= | kwa kichwa |
| (iii) | Mbuzi.......................................... | 500/= | kwa kichwa |
| (iv) | Kondoo.......................................... | 500/= | kwa kichwa |

Ada ya huduma nyingine

(i) Ada ya ukaguzi wa gari la kubebea nyama 5,000/= kwa mwezi

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S.

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 180 la tarehe 18/05/2012

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA (KILIMO CHA MAZAO YANAYOSTAHIMILI UKAME) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kilimo cha Mazao Yanayostahimili Ukame) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Eneo la matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa Kilimo pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Ghala" maana yake ni chombo, chumba, kifaa chochote cha asili au sehemu maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya kuhifadhi chakula;

"Mkazi" maana yake ni mtu yeyote wa kawaida anayeishi katika eneo la Halmashauri isipokuwa mtu yeyote:-

(a) mwenye umri chini ya miaka 18;
(b) asiyejiweza kutokana na ulemavu, kuugua au uzee;
(c) mwanafunzi aliyeko masomoni muda wote.

"Mazao" maana yake ni mimea inayopandwa mashambani kwa ajili ya kuzalisha chakula au malighafi kwa ajili ya biashara;

"Mazao yanayostahimili ukame" maana yake ni mazao yanayolimwa na kustawi vizuri katika sehemu zenye uhaba wa mvua au ukame.

Wajibu wa kulima

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi wa Halmashauri kufuata ushauri wa kitaalam atakaopewa na Afisa Muidhiniwa na kuhakikisha analima na kuendeleza:-

(a) ekari mbili za mazao yanayohimili ukame;
(b) ekari moja ya mihogo;
(c) ekari mbili za mazao mengine ya chakula na biashara.

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa

5. Afisa muidhiniwa anaweza kuingia wakati wowote kwenye eneo au shamba wakati wa saa za kazi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kuhifadhi chakula

6. Itakuwa ni jukumu la kila mkazi hususani mkuu wa kaya kuhakikisha kwamba anahifadhi chakula cha kutosha yeye na familia yake kwa angalau miaka miwili au zaidi.

Wajibu wa kaya

7. Itakuwa ni jukumu la kila kaya kuhakikisha kuwa:-

(a) wana ghala la kuhifadhi chakula; na
(b) ghala hilo linakuwa katika hali ya usalama na kwamba hakuna uwezekano wa chakula hicho kuharibika;
(c) wanadhibiti wadudu wanaoharibu chakula kama vile dumuzi, panya.

Makosa na adhabu

8. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

9. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

JEDWALI

SHERIA NDOGO ZA (KILIMO CHA MAZAO YANAYOSTAHIMILI UKAME) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2011

HATI YA KUKIRI KOSA

*(Chini ya kifungu cha 11)*

Mimi.........................................................................................nakiri mbele ya .....................................Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, kwamba mnamo tarehe..........................ya mwezi .................. mwaka ...................... nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ............ cha Sheria Ndogo za (Kilimo cha Mazao Yanayostahimili Ukame) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2011. Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza Mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

*Tarehe*.................................. *Sahihi*............................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12 mwezi Agosti 2011 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S.

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI

Dodoma,
21 Aprili, 2012

MIZENGO P. PINDA (MB),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 181 La tarehe 18/05/2012

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha. 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KITUO CHA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali. Jina na tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Eneo la kutumika

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri

"Abiria" maana yake ni mtu anayekuwepo katika kituo cha basi kwa madhumuni ya kupata usafiri wa kumpeleka sehemu nyingine;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Gari" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, pikipiki au wanyama wanaotumika kama chombo cha usafiri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo;

"Kibali" maana yake ni ruhusa ya kufanya shughuli yoyote ambayo hutolewa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi;

"Kituo cha magari" maana yake ni neno lolote lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kushusha abiria na mizigo pamoja na sehemu za minada, magulio, mialo au masoko ambapo magari hupakia na kushusha abiria na mizigo;

"Mabasi" maana yake ni mabasi yanayofanya safari zake kwenda na kutoka mikoa mbalimbali na maeneo mengine ndani ya Halmashauri;

"Maegesho" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa na Halmashauri

kwa ajili ya kuegesha magari;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mmiliki" maana yake ni kondakta, dereva anayetumia gari kwenye maeneo ya stendi;

"Ushuru" maana yake ni malipo yanayofanywa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa kuingia stendi

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa magari ya abiria na mizigo yatokayo yanakwenda Mikoani na maeneo yaliyo ndani ya Halmashauri kuingia katika eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa magari ya abiria na mizigo kama inavyoonyeshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ushuru huo utalipwa wakati gari linapotoka stendi kuanza au kuendelea na safari zake.

Wajibu wa kulipa Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari la abiria au mizigo kulipa ushuru kama ilivyoelekezwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Afisa Muidhiniwa au wakala ambaye atatoa stakabadhi inayolingana na malipo yaliyofanyika.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu atakayelipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi kutoa risiti.

Ulipaji wa Ushuru

6.-(1) Mmiliki yeyote atakayeshindwa au kukataa kulipa ushuru katika muda anaotakiwa kulipa Halmashauri inaweza kukusanya ushuru huo kwa njia ya polisi au mahakama.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 6(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata gari lolote la mizigo au abiria na kulishikilia mpaka

utaratibu wa kulipa ushuru unaodaiwa utakapokamilika.

(3) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote itakayotokea ama wakati wa kukusanya ushuru au kwa gari lililokamatwa na kushikiliwa pamoja na mali zilizo ndani ya gari.

7.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mmiliki yeyote:- Usimamizi wa maegesho

(a) kuegesha au kulaza gari kwenye maeneo ya barabara;

(b) kufanya matengenezo makubwa au madogo au kuosha gari ndani ya stendi.

(2) Wamiliki wote watatakiwa kuegesha magari yao katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

8. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari la abiria kuhakikisha kwamba gari lake lina kibao cha safari kinachoonyesha mahali ambako gari linapotoka na linapokwenda. Kibao cha safari

9. Itakuwa ni makosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:- Makosa

(a) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;

(b) ataosha gari au kufanya matengenezo makubwa ndani ya stendi au kituo cha mizigo;

(c) atasababisha au kufanya fujo ndani ya eneo la stendi;

(d) atatumia lugha mbaya ndani ya eneo la stendi;

(e) atatupa takataka hovyo kwenye eneo la stendi;

(f) atapakia abiria au mizigo katika sehemu isiyo ruhusiwa;

(g) atazuia watumiaji wengine wa stendi kutumia kwa njia yoyote ile;

(h) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake;

(i) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru.

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote atakayekiuka kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi na Mkosaji atakiri kosa na kukubali kulipa faini isiyozidi ile iliyoainishwa katika kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI I

USHURU WA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO

| Na. | Aina ya Gari | Ushuru (Tsh) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabasi makubwa (Abiria 45 na zaidi) | 3,000 | Kwa siku |
| 2. | Mabasi madogo (chini ya abiria 45) | 2,000 | Kwa siku |
| 3. | Taxi, Pick-up, station wagon | 1,000 | Kwa siku |
| 4. | Malori | 3,000 | Kwa siku |
| 5. | Kulaza gari kituoni | 2,000 | Kwa siku |

JEDWALI II

USHURU WA MAEGESHO

| Na. | Aina ya Gari | Kiasi kwa siku |
|---|---|---|
| 1. | Gari la mizigo | 2,000/= |
| 2. | Station wagon | 1,000/= |
| 3. | Taxi | 500/= |
| 4. | Pikipiki | 500/= |

JEDWALI III

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KITUO CHA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2011

Mimi..........................................................Nakiri mbele ya...........................................

......................................................................Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

ya wilaya ya Urambo kwamba mnamo tarehe............ya mwezi wa..........................

mwaka...............Nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha.....................

..........................Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2011. Nipo tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi atatekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni yangu ya kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.......................................................     Sahihi...............................

TANGAZO LA SERIKALI NA. 182 LA tarehe 18/05/2012

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA YA WILAYA
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha. 153)*

SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA ZA HALMASHAURI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO, 2012

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo (Utunzaji wa barabara za Halmashauri) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Eneo la matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mhandisi wa ujenzi au Afisa yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

"Barabara" maana yake ni barabara zote zinazopitika kwa magari katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya;

"eneo la barabara" maana yake ni eneo la barabara lililohifadhiwa ambalo ni umbali wa meta kumi na tano (15) kila upande kutoka katikati ya barabara;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo;

"Kijiji" maana yake ni kijiji kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya);

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

4.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba:- Wajibu wa Halmashauri

(a) barabara zote zilizoko kwenye eneo lake zinapitika kwa kipindi cha mwaka mzima;

(b) magari yanayopita katika barabara hizo ni yale yanakubalika kulingana na uzito unaotakiwa;

(c) itatenga njia maalumu za kupitisha mifugo (cattle track) wakati wa kwenda na kurudi malishoni na minadani au mahali pengine;

(d) inaendeleza na kutunza barabara zote kwa kuzifanyia ukarabati wa mara kwa mara.

Kulima au kujenga kwenye maeneo ya barabara

5.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mkazi yeyote kujenga au kulima kwenye maeneo ya hifadhi za barabara.

(2) Halmashauri itampa notisi ya siku thelathini (30) mkazi yeyote aliyejenga au kulima kwenye maeneo ya hifadhi ikimtaka kubomoa jengo au kung'oa mazao aliyopanda katika maeneo ya hifadhi ya barabara.

(3) Endapo mhusika atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu cha (2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubomoa jengo hilo au kung'oa mazao yaliyopandwa na kumtaka mhusika kulipa gharama zote ambazo Halmashauri itakuwa imeingia.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mkazi yeyote:-

(a) kuharibu miundo mbinu iliyowekwa na Halmashauri;

(b) kupitisha mifugo yake kwenye barabara iliyohifadhiwa.

(5) Kila mkazi anayetaka kupitisha mifugo yake ndani ya barabara iliyohifadhiwa atatakiwa kuomba kibali cha kupitisha mifugo hiyo kutoka Halmashauri.

Makosa

6. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote:-

(a) kujenga nyumba au kuchimba mchanga kwenye maeneo ya barabara;

(b) kuelekeza maji kwenye maeneo ya barabara;

(c) kupitisha mifugo kwenye maeneo yote ya barabara na hifadhi zake;

(d) kuharibu alama za barabara;

(e) kukata barabara bila kibali cha Halmashauri;

(f) kutupa takataka kwenye barabara au mitaro;

(g) kutengeneza gari akiwa kandokando ya barabara;

(h) kutengeneza gari akiwa ndani ya barabara bila kibali.

Adhabu

7. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

8. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA ZA HALMASHAURI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2012

HATI YA KUKIRI KOSA

*(Chini ya Kifungu cha 8)*

Mimi.........................................................nakiri mbele ya..........................................

........................................................................Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

ya wilaya ya Urambo kwamba mnamo tarehe............ya mwezi wa...........................

mwaka...............Nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha...................

..........................Sheria Ndogo za (Utunzaji wa Barabara za Halmashauri) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012. Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza Mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....................................................          Sahihi...............................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 12/8/2011 na nembo hiyo imebandikwa mbele ya:

JUSTUS M. MOLAI,
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Urambo*

L.S.

ADAM MALUNKWI,
*Mwenyekiti wa Halmashauri (W)*
*Wilaya ya Urambo*

NAKUBALI,

Dodoma,
21 Aprili, 2011

MHE. MIZENGO PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 183 la tarehe 18/5/2012

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA, 2012

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Vibao vya Matangazo ya Biashara) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Eneo la matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo: Tafsiri

"Afisa Muidhinishwa" maana yake ni pamoja na Afisa Biashara wa Halmashauri na Afisa ye yote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Urambo;

"matangazo" maana yake ni maandishi yo yote yaliyoandikwa au kubandikwa kwenye vibao au ukuta wa Jengo au chombo cho chote kwa ajili ya kutangaza biashara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, pamoja na Afisa ye yote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"vibao vya matangazo" maana yake ni mbao, ukuta au mahali po pote na chombo cho chote ambacho kimewekwa kueleza biashara inayoendeshwa kwenye eneo husika.

4.—(1) Halmashauri itatoa ushuru vibao vya matangazo yatakayobandikwa katika sehemu yo yote ya Halmashauri kwa viwango vilivyoonyeshwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi isipokuwa kwa matangazo ya Serikali na Taasisi zake. Ushuru

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara kuweka kibao cha kutangaza biashara yake na atatakiwa kulipa ada ya kibao hicho kwa viwango vilivyoainishwa na Halmashauri.

Muda wa kulipa ushuru

(3) Matangazo ya biashara yatalipiwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Serikali isipokuwa kwa matangazo yatakayovumishwa kwa vipaza sauti pamoja na matangazo ya vitambaa ambayo yatalipiwa wakati wa kuombewa kibali.

Ukaguzi

5. Mkurugenzi au Afisa Muidhinishwa anaweza, kwa wakati wo wote kufanya ukaguzi katika eneo la biashara na kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Uwezo wa Afisa Muidhinishwa

6.–(1) Afisa Muidhiniwa anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa mfanyabiashara ye yote ambaye atashindwa kulipa ushuru wa vibao vya matangazo chini ya Sheria Ndogo hizi kumtaka alipe ada hiyo katika muda utakaoneshwa katika taarifa hiyo.

(2) Endapo mfanya biashara ye yote atashindwa kulipa ushuru katika muda uliopangwa, Afisa Muidhinishwa anaweza kuondoa tangazo hilo na kudai gharama za kuondoa tangazo hilo kutoka kwa mfanyabiashara huyo.

(3) Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lo lote wakati wa saa za kazi kufanya ukaguzi kuona utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

7. Mtu ye yote atakayepuuza au kukataa kulipa ushuru atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi sita au adhabu zote yaani faini na kifungo kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

8. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyozidi shilingi elfu hamsini mtu ye yote endapo mkosaji atakiri kutenda kosa hilo kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoko kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

| *Na.* | *Aina ya Tangazo* | *Kiasi cha Ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Matangazo ambayo yataandikwa kwenye vibao na kubandikwa sehemu za wazi kwenye eneo la mji | |
| | (a) Matangazo yasiyotoa mwanga | 4,000/= kwa mwaka |
| | (b) Matangazo yanayotoa mwanga | 5,000/= kwa mita kwa mwaka |
| 2. | Matangazo ambayo yataandikwa na kuwekwa Vijijini na nje ya mji | |
| | (a) Matangazo yasiyotoa mwanga | 2,000/= kwa mwaka |
| | (b) Matangazo yanayotoa mwanga | 3,000/= kwa mwaka |

| *Na.* | *Aina ya Tangazo* | *Kiasi cha Ushuru* |
|---|---|---|
| 3. | Matangazo yatakayoandikwa na kuwekwa kwenye nyumba za biashara juu ya mlango | |
| | (a) Matangazo yasiyotoa mwanga | 2,000/= kwa mwaka |
| | (b) Matangazo yanayotoa mwanga | 3,000/= kwa mwaka |
| 4. | Matangazo yatakayobandikwa kwenye magari | 3,000/= kwa mwaka |
| 5. | Matangazo kwa njia za nyimbo au kipaza sauti | 20,000/= kwa siku |
| 6. | Matangazo ya kutumia vitambaa (cloth banners) | |
| | (a) Upande mmoja | 5,000/= kwa tangazo |
| | (b) Pande mbili | 10,000/= kwa tangazo |

## JEDWALI LA PILI

### SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO ZA MWAKA 2012

Mimi ........................................................ Nakiri mbele ya ..............................................

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwamba mnamo tarehe .......... ya

mwezi ................................ mwaka ................. Nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya

kifungu cha ................................... Sheria Ndogo za (Ushuru wa Vibao vya Matangazo ya Biashara) za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo za mwaka 2012. Nipo tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi atatekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe .................................................... Sahihi ..............................................................